

Title: NAMES OF GOD

By Dr. w. euGENE SCOTT, PhD Stanford University

Preached at the Los Angeles University Cathedral

Copyright © 2007 Pastor Melissa Scott – all rights reserved

Somo: MAJINA YA MUNGU

Imehubiriwa na Dk. w. euGENE SCOTT, Daktari wa Falsafa, Chuo Kikuu cha Stanford

Katika Kanisa Kuu la Chuo Kikuu cha Los Angeles

Haki © 2007, Mjungaji Melissa Scott. – Haki zote zimehifadhiwa

MAJINA YA MUNGU

Ukishatoka hapa leo, kusikiliza kwa mara ya 21 ujumbe huu ninaohubiri kila mwaka, najua hilo halitakuwa jambo la kutisha katika kona ya kuta za ubongo wako sehemu fulani, lakini itaendelea kuteremka kwenye maji maji ya mifupa ya maisha yako na uhusiano wako na Mungu na kukupeleka katika baadhi ya masumbufu ya 1996.

Na nitakupeleka kwenye Isaya 50, Agano la Kale: “Ni nani kati yenu” – na mara kulenga ujumbe huu kwako – “Ni nani kati yenu anayemugopa Bwana, anayetii sauti ya mtumishi wake?” Moja kwa moja tunajua kwamba hatujishughulishi na baadhi ya wakosefu wa kiroho, baadhi ya wakorofi. Tunajishughulisha na watu waomuhofu Bwana katika ule uasili wa neno: wanaheshimu, wanahofu, wanatambua ukuu wake na haki zake zote juu yetu sote. Hatujishughulishi na mtu asiyemwamnini. Tunajishughulisha na lile kundi la watu ambao kwa matumaini wanawakilishwa hapa leo.

“Ni nani kati yenu anayemugopa Bwana, anayetii sauti ya mtumishi wake?” Mara nyingine tena natumia hili neno, sio “mkosefu”. Mtu fulani anayejitahidi – unamhofu Bwana, unatii sauti ya mtumishi wake. Na ukisikia kweli ikihubiriwa, kama ukijisajili na macho kuona nuru, na ukitafuta kwenda nao sambamba – watu wazuri kama ninyi. Sasa, hakika hakuna mmoja wapo kati yenu leo hapa asiyemhofu Bwana, ambaye angalau asiyejaribu kumtii mtumishi wake, unajitahidi kutii. Kwa hiyo ujumbe huu unakufaa “anayetembea kwenye giza, hana nuru?”

Sasa, umeshakuwa hapa pamoja nami kwa mara 20. Kijana, nilijua kweli ya hili jambo mwaka jana. Unakwenda, mara ghafla nuru inatoweka na huoni njia upande wowote. Na hujui ujumbe huu umelegwa kwa na leo hii, lakini popote ulipokaa; unasikiliza runinga, unasikiliza redio kuhusu habari za kimataifa; nina hakika kuna haya wataki huu, yaliyojificha – yawezekana hayaonekani katika muonekano wa sura zao kama njia ya kujiweka jasiri – lakini, sikiliza unatembea katika giza, na huwezi kuiona nuru. Mgandamizo wowote – mgandamizo wa tukio, kifedha, afya, uwapendao, kuvunjika kwa mahusiano, idadi yoyote ya mambo ya giza yanayokusonga, hupati sababu ya jambo lolote ulilolifanya kukuelezea giza. Uko tu ndani ya giza hilo, na linakumeza. Na kama huko hapa leo, ninataka kukuambia kitu fulani: itakugonga hata kabla mwaka haujaanza – msemu wa maarufu, , “Wafurahishe watakatifu, mambo yatakuwa mabaya.”

Sasa sitaki kuendelea na ujumbe labda nijue kwamba tuko pamoja. Unafahamu ninachokiongea? Oh ninajua, wahubiri wengi wa Kikristo wanosema kama ukimtumikia kwa udhahiri, haya mambo hayawezi kukukuta. “Dada Sals” na “Kaka Jimmys” wanainyooshea kidole na kusema – kama vile nimemtaja mtu fulani kuwa yuko gizani, natavuta wenye haki kanzu zao, kanzu za wanojihesabia haki nyuma yenu na mtaona maswali kwenye macho yao, “Vema, ni kitu gain ulichokosea mpaka mambo

haya yanakutokea?” Hili giza linamfungii mtu “ambaye anayemuhofu Bwana, anayetii sauti ya mtumishi wake”, kisha anatembea katika giza na hana nuru.”

“Vema, ni nini tunachotakiwa kufanya kuhusu hili? Ni wangapi waotaka kuondoka kwa sababu ya ujumbe huu hauna jambo lolote linalokuhusu? Nyoosha mkono wako juu kwa sababu nataka kukusindikiza ukitoka nje. Ni watu wangapi – nitakaowauliza kwa mara ya pili – kujua ninachoongelea? Giza.... Na kila wakati kuna mawazo ya chini chini, “Nimefanya nini cha ajabu,” kama tunavyosumbuka. Vema, ngoja ni kuambie kitu cha kufanya?”

Mstari wa kumi na moja. Nitauachia kwa haraka ujumbe huu kwa sababu ni ule unaotakiwa kutenda. “Tazama, moto wote uwakao, unaokuzunguka na kukumulika: tembea katika nuru ya moto, na miale uliyoiwasha. Hii itakuwa na mkono wangu; utalala chini kwa huzuni.” Ninataka kuuachilia na hii upesi kama nikiweza kwa sababu ni ngumu ku...., kwa sababu ni wazi tunavyokuja juu wakati wa vipingamizi vinapokuja njiani na kwenye giza linalokuja. Ninajua jinsi Gene Scott amefanya hivi kwa miaka.

Wale wanaonijua vema na wako karibu yangu labda wanaweza kucheka kuhusu hili jambo, kwa sababu ninavuta kiko na ninavuta sigara na ninaanza kupata aina fulani ya nuru, kiko kidogo kama kalamu ya risasi kimewaka miaka iliyopita kutoka kwa marafiki wanaoniletea tumbaku na sigara. Hii ni kati ya mambo yanayoudhi uliyowahi kukutana nayo. Watatoka na wewe kwa ajili ya maongezi pale unapowahitaji sana. Ni kama kalamu ndogo za risasi..., natamani kama ningekuwa na mojawapo— angalia, sijawahi kuwanao hata kama nikiwahitaji. Nitawabeba wanne au watano, na kama nikitaka kufanya jambo kubwa la mguso kwa kuvuta hiki kiwashio nje, ninachaganyikwa na ninataka kurudi nyuma kuizungusha BIC yangu! Haya mambo hayakushindi.

Hivyo wanaonijua mimi vema watacheka kuhusu jambo hili kwa sababu ninakwenda kuelezea mwenenondo wangu katika lugha ya kimaumbo. Wakati giza likija, ninawasha kibiriti upesi kuliko mtu mwingine yeyote, ni lugha gani ya kimaumbo ninayoiongelea. Unajua, nina mtu anayenifanyia kazi – anaelezeza jinsi nilivyokuwa na mahusiano na Mungu kwa miaka. Ndiyo maana natambua hilo kwa upesi sana – “inamchukua mtu kumfahamu mtu”. Huyu ni mtu anayenifanyia kazi – nitakueleza hadithi moja nzuri.

Tulienda nyumbani kwangu kupitia Ziwa Almanor. Tuna gari kule uwanja wa ndege. Tulikuwa wa kwanza wakati wa majira ya vuli kufungua nyumba, ninajua hakutajuwa na vitu vya kutumia nyumbani. Tunasimama katika mojawapo.... Gari lenyewe ni moja ya magari ya ajabu yanayosimama bila kujali hali ya hewa. Unaweza kuliacha kwenye theruji ipatayo kina cha miguu 10 na kisha kulichimbua na kuliwasha. Siku hizi hawatengenezi magari ya jinsi hiyo tena. Ni aina ya zamani ya station wagon lakini inawaka.

...Hivyo tunaingia kwenye station wagon pamoja na jamaa zangu waliokuja kunisaidia kufungua nyumba na tunaendesha kwenda Chester, mji mdogo labda maili moja kutoka uwanja wa ndege, kabla ya kwenda nyumbani kwangu. Na tuko kwenye kituo cha gesi kujaza mafuta gari na najua hatuna vitu vya matumizi nyumbani, hivyo nasema – nimuite nani? Sitaki kumtaja jina. Kuna jina ninaloweza kulitumia? Simjui mtu yeyote anayeitwa Yakobo, hivyo tumuite Yakobo, ingawa kila moja anayefanya kazi pamoja nami anajua ni yule ni nani. “Yakobo....” Sasa kuna duka la vitu hapa mtaani. Ni barabara kuu nne inayopita kuelekea chini, magari yanakuja na kuondoka, na kwa upande mwingine tupo katika kituo cha matengenezo ya magari. Nasema ”Yakobo nenda kule kwenye duka....”(Na nilikuwa nataka kusema, “kalete vitu vifuatavyo”), lakini ninavyosema “nenda”, anaanza kwenda; na niniliposema “kule kwenye duka”, alikuwa akielekea upande ule, na muda nilipofika mwisho wa sentensi, alikuwa upande

mwingine wa barabara. Alikuwa hana wazo la kitu gani nikichotaka anunue pale dukani, lakini alikuwa akielekea dukani.

Huyo ni mimi na Mungu. Huyo ni Yakobo katika Agano la kale. Hakuna kitu chochote kibaya Yakobo alichotaka kufanya. Mungu aliweka wazi mbele ya Yakobo na Esau walipozaliwa: “Nimempenda Yakobo; Nimemchukia Esau.” Lakini Yakobo alijiweka vizuri kufanya mapenzi ya Mungu kwa nguvu zake. Hakumsubiri Mungu kufanyia kazi. Alipo ... na alipoungana na mama yake katika ule mpango, wao wawili walipata picha ya jinsi ya kufanya kazi ya Mungu ifanyike kabla Mungu hajafika pale. Jina lake ni “mshika – kisigino.” Alitoka tumboni akishika kisigino cha Esau. Esau alizaliwa kwanza na alikafatia Yakobo, akimshika kisigino cha Esau. Katika mawazo ya Yakobo, Esau hakutakiwa kuzaliwa kwanza. Walishindana tumboni: “Na kwa Mungu, nitafanya iwe vigumu kutoka!” Hii ndiyo hadithi ya maisha mpaka ailpokata kamba, akitoka kuangalia muziki katika usiku mmoja maarufu alishindana usiku mzima na malaika, mwishowe akawa kilema pale malaika alipomgusa paja lake na hakumrudishia tena. Alichofanya ni kumsubiri. Na kisha malaika akabadilisha asili yake, akalibadilisha jina kutoka Yakobo kuwa “mshika – kisigino” kuwa “Israeli”: “mwana aliye na nguvu za Mungu; lakini kwa hakika, inamaanisha *El*, au “Mungu-anayeongoza”. Kuongozwa na Mungu – nguvu mpya ilikuwa pamoja naye. Hiki ndicho kinachosemwa hapa.

Giza lolote unalokutana nalo, kitu cha kwanza ni kutatua tatizo peke yetu – kuanza kusugua njiti za vibiriti, kuwasha moto, kuwasha moto kufukuza giza – si kwa kutumia kitu chochote bali akili alizotupa Mungu na kwenda mbele zaidi ya Mungu ili kutatua tatizo tulilonalo. Nimekuwa nikihubiri hivi kwa wiki nyingi zilizopita. Unajitoa kwa Bwana, unatulia na kusubiri wa saburi. Kilichoahidiwa hapa ni hakika. Haijalishi ni jinsi gani ulivyojitoa kwa Mungu, jinsi gani wewe ni mwema, jinsi gani unavyojitahidi kuenenda sawa; baadhi ya safari yako itachangamana na giza – mambo fulani yanayokuzunguka na kukuzinga macho yako kuona. Na kama ukianza kupeperuka, ukijenga moto wako – vitu vyako vya mwili vya ukombozi, akili yako kama ni njia pekee ya ufumbuzi wa matatizo, kama ukianza kwenda kila upande kwa mara moja, kuvuka barabara kuelekea kwenye duka kabla hujajua Mungu anachotaka kukuambia, kisha utaenda “kwenye nuru ya moto wako mwenyewe”. Utapata nuru zaidi na zaidi ulioitengeneza mwenyewe. Na “kujilaza chini kwa huzuni.” Sifahamu ni jinsi gani niliweke hili kwa uwazi. Sihubiri ujumbe wote kuhusu hili.

Ni kujjenga katika maisha ya Kikristo – kwa wale walioamini uwepo wa Mungu pamoja nasi asiyeonekana kila wakati – ni kujiungamanisha... katika njia ya Yakobo au ule ukimya. Nimesema hivi kwa miaka 20, weka vibiriti nje kidogo mpaka upate nguvu kidogo kuanza kuwasha moto wako. Ninazungumza lunga ya kimafumbo. Ukristo sio maisha ambayo tunaongozwa na Mungu kama vile mbeba mizigo wakati fulani wakati sisi wenyewe hatuwezi kufanya hivyo. Ukristo ni njia, ni matembezi, ni safari. Ni mwenendo wa maisha unaotambua na kukupa uwepo usioonekana kwa macho ya kawaida. Mungu yuko pale kila wakati. Huna haja ya kuhaidi ile kuwa katika uwepo wake. Lakini, kama dunia, mwili, na shetani watatuzunguka, watatuteka, watatutawala; Roho wa Mungu ni Roho mpole. Yeye hakisii. Hatawasaidia wale wasiomwalika. Yeye hapendi mtu anayejitumainia, kama unataka kung’ang’ania vibiriti vyako, kutatua matatizo yako, kujenga moto wako, kuleta giza lako. Atakuambia. Na hivi ndivyo wengi wenu wamekuwa wakifanya; na hivi ndivyo Gene Scott mara nyingi, lakini nakuwa mwerevu.

Weka kibiriti mbali! Yakobo alikwenda kwa kuchechemea kwa maisha yake yote akimkumbusha yeye kwamba alikuwa ni Mungu anayeongoza. Mwacheni Mungu apange risasi badala ya kufanya uharibifu ambao anaweza kuurekebisha. Hiyo siyo njia ya kujitoa katika giza. Giza linakuja. Ni nini cha kufanya? Ninyi, msikilizeni Mungu. Kama haneni, endelea mbele na washa kibiriti. Lakini acha

kujisumbukia, kuzunguka kwenye magurugumu, hofu, wasi wasi, kujikwamua wenyewe. Sitapoteza tena muda katika hili. Kama mpaka sasa hujanielewa, kwa heri!

Sasa unafanya nini tena kama huwezi kufanya hili? Vema, unakaa kimya sana kabla hujaanza kuwasha moto wako katikati ya giza lako ni kufanya yafuatayo: “Mwacheni alitumaini jina la BWANA.” Vema sasa, hiyo ni sentensi rahisi sana. Ngoja niielezee. “Mwacheni amtumaini yeye” —*ibeteh* ni neno la Kiebrania. Kwa kweli asili yake ni *beteh*. Maana yake “kumwachia Mungu kila kitu —kutokata tamaa mwenyewe kwa kiasi ambacho wakati fulani unaweza ukapata picha ya kuwa unajinamia mwenyewe mbele ya mtu. Ni moja ya maneno mazuri ya Kiebrania ya kuelezea tabia halisi mbele za Mungu wakati wa uhitaji. “Mwacheni mwenyewe ainamishe uso chini” kama utaweza “fanya kwa Mungu”. Hii ni rahisi naona kama ninaudhihakia uelewa wako. Lakini ni mambo madogo tunayoyakosa.

“Oh, niko gizani!” Sugua, sugua, sugua, sugua. “Kiko wapi... kiko wapi kifaa changu cha kuwashia moto? Giza linakuja. Washa na utafute kwa utulivu, maombi yasiyo na msaada ya nini? “Katika jina la Bwana” Yakikusanya kila kitu katikati, yakikusanya giza, funika giza lenyewe katikati, kwa mwitikio mbaya, ninaruka mwenyewe kwa nini? “Jina la Bwana.”

Hapa sasa ninapata theologia nzito, lakini sentensi inakosa maana: “Majina ya Bwana.” Kwa nini majina mengi? Tunaanzia mwanzo. Hapo mwanzo *Elohim* aliziumba mbingu na nchi.—hilo neno la ajabu kwa kinyume na kwa Kiebrania linasomwa kutoka kulia kwenda kushoto lakini likageuzwa kwa Kiingereza na kuitwa *El*, “Aliye Juu”. Maana ya kwanza ya jina la Mungu —“ Aliye Juu”, juu ya kila kitu na katika wingi kwa kuanza na Mwanzo. “Hapo *Elohim*, yeye Aliye Juu; Mungu —“ aliziumba mbingu na nchi”. Lakini unakuja kwenye watu Mungu aliowachagua, Abram. Na kisha Mungu anaanza kuongeza neno *El* maneno mengine. Una *El* na zaidi. *Elolam—Elolam* maana yake ‘Aliye Juu Sana’, Mungu Aliye Juu— kama Aliye Juu halitoshi, “Aliye Juu Kuliko vyote”.

El Shaddai—Nilihubiri katika siku ya kina mama; kwa kweli, “wanaonyonyesha”. Ni picha ya mama akimnyonyesha mtoto kwenye matiti yake na akimpatia mahitaji yake yote. Na haya majina yanazidi kuja kama Mungu akiyafunua mwenyewe kwa mtu fulani anayemwamini, Abram — Mungu alichamchagua yeye kati ya watu wote wa duniani kuwa mfano wa Ufunuo wake kwa yeye mwenyewe.

Na kisha unakuja ufunuo mkubwa wa Israeli—watu waliongozwa na Musa, na mwisho wakapokea mafunuo yote kwenye mlima Sinai. Lakini Mungu anasema, “Nimekuwa nikijulikana kwa Jina Langu *El*”—‘Aliye Juu’—“lakini sasa nitajidhihirisha Mwenyewe kama *Yahweh*, kama Jehovah (Yehova)” — jina lingine la Mungu ambalo ni maarufu katika mabadiliko ambapo Wasomi wengine wa Biblia wanajaribu kuwa na maandishi wawili tofauti wakinakili hii torati ya awali katika vipengele vya Biblia, kwa sababu mmoja anamuabudu *El* na mwingine anamuabudu Jehovah (Yehova) au *Yahweh*. Hapana! Ni Mungu yule yule anayeukuza ufunuo wake kwa watu na anafanya kwa majina. Majina yanamaisha kitu fulani, sio tu misamiati isiyojipanga vizuri. Kama anavyofunua sifa, kisha anaelezea kwa sifa na kuongeza jina lake mwenyewe la kudumu. Na kwa hivyo inakuwa maandiko ya kisasa ya Kiebrania, *Yahweh*. Hizi herufi kubwa nne katika hili neno—ya-ha-wa-h, Y-H-W-H; na... (kwa sababu Wajerumani hawakuweza kutamka herufi “w” na ikawa herufi “v”), na likaandikwa kwa Kiingereza kutoka *Yahweh* kwenda Jehovah (Yehova), lakini kwa asili ni herufi nne zilizoandikwa kutoka Kiebrania: Yod-He-Vav (au Wav) na —ni. *Yahweh*, Jehovah (Yehova).

Sasa nimeshakwambia kwamba Kiebrania ni lugha yenye kutumia picha. Ni ipi picha ya Yehova? Kutoka “Yeye Aliye Juu” ambaye unamtazama na unapata sifa zake. “Nitajidhihirisha mwenyewe kama Yehova”. Maneno yenye mtazamo wa picha yanajidhihirisha wazi, ingawa hayakuwa hivyo neno alipokuja, lakini ni mfano mzuri wa kisasa uliobeba jina la Yehova. Angalia pamoja na nami katika

theolojia; fikiria kama vile umekamata bomba. Umeshawahi kukamata bomba na kugeuza maji kwa kufinya mkono—unahisi mgandamizo ukiongezeka? Hivyo ni sawa na ninavyokuja kukupa kwa kifupi picha ya jina la Yehova. Ni kama vile asili ya Mungu inatoa mgandamizo kama wa maji katika bomba lillilofinywa kutoa na kupulizia au kuleta manufaa yake. Hilo ndilo jina Yehova – Mungu mgandamizo wake uko katika ufunuo.

Na kwa watu aliowachagua kama ufunuo wake ulioandaliwa na Mungu kuwa sauti ambayo itaiambia dunia kuhusu Mungu, anasema, “nitajidhihirisha mwenyewe”, sio kama *El*, “Aliye Juu” na juu pale, lakini kama “Yehova akitafuta kuja na kujidhihirisha mwenyewe kwenu.”

Ni janga kubwa ambalo Shetani amelileta kinyume na mpango wa Mungu uliotokea kati ya watu wake walioitwa wenyewe kwa sababu wasomi walileta mawazo ya kitoto yaliyopendekezwa na upagani kwamba Yehova liwe jina juu ya mwanadamu haikuweza hata kutamkikwa. Hivyo wakisoma maandiko, kakika ile tafsiri ya *King James* ukiona “BWANA” kwa herufi kubwa, jua kwamba inatafsiri ya *Yahweh*, Jehova.

Lakini kwa namna ya asili ya kuabudu ya Kiebrania, waliposoma maandiko walikwenda kwa Yehova, walimuita *Adonai* au kwa maneno mengine ni “BWANA”. Hawakutamka “Yehova”. Waliifanya kuwa nchi ya siri. Wakati Mungu alitaka jina lake kuwa lidhihirishwe kama yeye jinsi alivyotaka yeye mwenyewe, na kwa kwake yeye na kupitia Yehova – ikiwa na *El* na luongezewa na *Shaddai*, Yehova anakuja kama maji katika bomba lilofinywa akijidhihirisha mwenyewe kwa watu wale wenye muonekano fulani kwa ajili ya mahitaji maalumu.

Na sasa niko katika somo la kuganga. Sijui giza lako ni nini, lakini Yehova katika maandiko yote ameongeza: Yehova- “mfano maalumu”. Katika giza lako na langu tunakutana na jina lenye maelezo ambalo ni ufunuo wa Mungu anavyotaka kuwa kwetu na imani ikamate na kusema hilo linakidhi mahitaji yangu. James Dunn aliwahi kusema Mungu ni kama mti mkubwa; kuna tawi la kila mmoja. Sipendi kujumuisha mahubiri yasiyotugusa pale tunapoishi na kupitia theolojia fulani nzito na lugha za Kibiblia tumefikia kwenye jibu la giza ni nini. Katika giza langu ambapo hakuna nuru, sitii shaka kile Mungu alichosema kwenye nuru; na mimi katika giza langu, badala ya kufanya nuru yangu kama kitendo cha kwanza, ni bora niende kwenye majina ya Mungu na nione kama kuna moja linakidhi hali yangu.

Vema, umesema lako ni tatizo la kiuchumi—Yehova-Yire. Nilianza kusema nawahubiria watu wenye imani, waumini wanaotii sauti ya Mtumishi wake. Ni giza la kifedha—giza lako, unaona njia yoyote ya kujikwamua? Vema, kabla hujaendelea na kutafuta juisi ambayo itakupa nguvu kwa aslimia 33% kwa siku—labda kabla hujawasha kiriti chako, kikiharibu sura yako ukifungua mdomo, ukijinyenyekeza na kumuomba Mungu msaada wake, unaweza ukafikia giza—japo huoni, Mungu anakuona—na anasema, “wewe, subiri kidogo! ‘BWANA atafanya’: Yehova-Yire.” Hii ndiyo maana ya hili neno.

Tunasehemu iliyopakwa rangi pale ukumbini. Zawadi kubwa Mungu aliyompa Ibrahimu, Mungu alisema, “ninamtwaa. Mchukue mpaka pale mlimani na umtoe kama sadaka ya kuteketezwa.” Chini ya kile mlima, Isaka anasema, “naona moto; ninaona kila kitu pia; iko wapi sadaka ya kuteketezwa?”—bila kujua kwamba angekuwa sadaka ya kuteketezwa.

Ibrahimu anasema, walipokuwa wanawaacha watumishi katika mlima, yeye na Isaka waliuandaa mlima, ni neno dogo tu watu wanalilikosa: “Tutarejea.”; sio “Nitarejea.” Hiyo ndio maana Ibrahimu anapata ahadi kubwa kutoka kwa Mungu katika ule wakati; na ndiyo maana ya alama ya pale ukumbini. Ibrahimu alifikia wakati kwamba angeweza kumwamini Mungu kwa kiwango cha juu kwamba, ingawa

huyu alikuwa mwana wa ahadi, mbegu aliyoisubiria maisha yake yote kuipokea; kama angemtii Mungu na kutumtoa sadaka ya kuteketezwa, Mungu angeweza kumfufua katika wafu. Isaka ulikuwa muujiza uliokuja kwanza; ungekuwa muujiza mwingine kama angefufuka katika wafu. Ibrahimu hakuwa na shaka; yeye na Isaka wangeshuka chini ya mlima. Na katika mfano huo linakuja jina la katika milima wa “Bwana itapatikana”.

Katika hali ya kutowezekana, imani inamkamata Ibrahimu na kusema: “Bwana atafanya.” Atafanya siku moja kwa wakati fulani. Sasa sifahamu ni nani aliye katika hilo giza, na uhitaji anaweza kuniambia kuhusu hilo; kabla hujaanza kuwasha vikibiriti vyako kuhusu hilo giza lako la kifedha, huu mstari unasema, “Liangalie jina la BWANA.” Na ikawa “Mtwike—litumaini jina la BWANA.” Haiko kwa herufi kubwa katika tafsiri ya *King James*? Yehova—Yehova-Yire.

“Vema, hili ni tatizo langu.” Labda ugonjwa wangu. Nitapiga kibodi kwa dakika chache asubuhi hii leo. Labda ugongwa unawasumbua wale uwapendao na unahangika kutafuta njia ya kuwakwamua kutoka kwenye tatizo hilo. Huna hata wazo ni mara ngapi umekuwa ukishugulika na hali ambazo madaktari wanasema, “Ni mwisho; hakuna kinachoweza kufanyika.” Mwisho wetu ni Mwanzo wa Mungu.

Au tatizo lako kati ya hili kusanyiko ni ugonjwa. Nina maana umepambana nao sana. Inaonekana kama hakuna njia, hakuna mwanga. Acha kila unachokifanya ili uweze kuchukua hatua ya imani kwa kujiachilia kwenye jina la Bwana—Yehova rapha. Baadhi ya hawa wacheza ngoma wanaodhihaki uponyaji wa asili wa Mungu kwa vipindi katika historia ya kanisa wamewageuza watu kutoka kwenye uponyaji wa asili wa Mungu. Lakini ilikuwa kwa watu wasiotii ambao walikuwa wakinung’unika katika jaribu la kwanza kule jangwani ambako Mungu alisema, “Mimi ni Yehova-rapha.”

Sasa ngoja nikuambie kitu fulani kuhusu majina ya Mungu. Wakati fulani Mungu anawaongoza watu hawa kwamba wawe unabii wake katika mfululizo wa matukio mpaka waufikie mwisho, wakiangalia na kuona jinsi Mungu alivyofanya. Kisha, kwa upole na makini—kwa sababu mambo yanayofanana yanatokea, Mungu akiyafanya mwenyewe—watatabiri jina lake. “Vema, Mungu yuko hivi.” Isaya alifanya hivyo alimwalia na alikwende zaidi ya mawazo yake, hadithi ndefu ya Mungu alishufghulika na watu wake. Isaya alisema; Mungu alifanya. Isaya alisema, “Hakika wewe ni Mungu ujifichaye nafsi yako.”

Lakini hapo mwanzo haya majina yalikuja moja kwa moja kutoka kwenye kinywa cha Bwana. Ni kama vile hakutaka kusubiri mpaka uzoefu wetu utufundishe sisi wenyewe. Aliacha dirisha wazi na kusema, “Hii ndiyo njia ilivyo; hivi ndivyo nitakavyokuwa.” Na anachagua wakati ambapo ni wa kutotii na anasema, “Ndimi”—hali fulani muhimu, sifa ya mtu; mtu hawezi kutofautishwa pasipo hii alama—“Mimi ni Yehova-rapha.”

Ninamkumbuka mwanasayansi mkubwa katika Chuo Kikuu cha Minnesota ambaye kwa muda wa miaka mingi alikuwa akitumiwa na Billy Graham kwenye mikutano yake kama ushuhuda wa maisha yake kama mwanasayansi ambaye hakuiacha imani yake kwa Mungu. Nimepata simu kutoka kwa George Otis akisema, “Gene, Fred yuko hospitali. Tumbo lake limeziba kabisa; anaelekea kufa kama wasipo mpasua na kutatua hilo tatizo, na nafikiri mtu wa kwenda na kuingea naye, kwa sababu ya uhusiano wa kitaluuma mlionao, ni wewe.” Sikusita. Nilipanda ndege kwenda Minnesota kuelekea Minneapolis. Nilikwenda na nikamuona Fred, na nilitumia muda wa saa moja naye... nikiwa pamoja naye Fred huku akijaribu kutafuta sababu kwa nini tusingeomba pamoja ili Mungu amponye. Mwishoni, kwa maudhi, nilisema, “Fred, Mungu haitaji sababu nyingine zaidi ya yeye alivyo, alisema ni sehemu ya asili yake. Hauhitaji vitu vingine vinanyotegemewa na watu wengine. Wewe na mimi (wawili)... Maandiko yanasema ‘Wawili wenu watakapokutana duniani katika jambo lo lote

watakaloliomba, kwa kuwa walipo wawili watatu kati yenu wekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.’ Fred, tunachotakiwa kufanya, ni kumuachia Mungu ajidhihirishe. Hatutakiwi kumwambia aponye. Hii ndiyo asili yake; Yeye ni Mungu mponyaji. Sielewi ukuu wake—hatuwezi tukachukua funguo za uzima kutoka kwenye mikono yake, lakini najua ninapoongelea kuhusu uponyaji, niko upande wake. Hakutuumba sisi tupate shida. Tunapokosea katika maisha yetu, tunaleta matatizo na shida zinakuja kama giza linavyokuja; lakini Mungu anasema kuhusu watakatifu, kifo kinapokuja, ‘Anachukua pumzi zao.’”

Mimi ni mmoja wa Wahubiri ambao... Nitasema: Utaenda kugombana na mimi kama ukisema kwamba mmoja wa watakatifu ni mgonjwa, ni wale ambao wakristo wa daraja la pili. Lakini, cha kushangaza, katika pumzi hizo hizo, nitasema kama giza lako ni ugonjwa, au po pote giza la ugonjwa linapokugusa, kabla ya kujaribu kulitatua mwenyewe, jiachilie mwenyewe kwenye jina hili. “Mungu, ulisema; ni asili yako. Nitakupa ufunuo halisi na uwe nuru ya giza lako.”

Naruka na ndege kutoka New York. Ninakuambia wewe huku juu ya mawingu—nyota, mwezi—kila kitu bado kinang’ara. Chini ya mawingu unaweza kusahau, lakini unatakiwa kukumbuka kwamba kule lule juu ya giza kwamba Mungu ni yule yule jana..., na leo..., na hata milele... na ujiachilie kwenye jina hili, kama giza lako ni ugonjwa.

“Vema, hili sio tatizo langu. Ninakaa hapa na wala sioni kama kuna thamani kuwa kwenye ibada kwa sababu ya dhambi.” Wote tunakwazika. Sasa, bila shaka, siielezei dhambi kama watu wenye imani kali wanavyofanya—ambacho ni kila kitu. Dhambi ni pale tunapogeuka kutoka kwenye njia ya Mungu. Na dhambi ni kupungukiwa, na jinsi unavyomkaribia Mungu ndivyo unavyokuwa na utashi mwepesi. Na wote tumepungukiwa ndiyo maana ule wimbo “Neema ya Ajabu” unakubalika dunia nzima; lakini kuna saa za giza zinazokuja. Hii ni kawaida. Na labda katika mlio wa sauti yangu kuna mwana mpotevu mwingine... au binti anayepigwa na giza la kupungukiwa, na upo gizani, hii ni tofauti. Ni aina inayotokea: unamuhofu Bwana, unaitii sauti ya mtumishi wake; lakini kati kati ya giza hukumu inakuja, kama Shetani mshitaki wa watu anavyokaa akitukumbusha mambo yetu ya zamani tuliyoafanya.

Yehova-tsidkenu. Natakwenda haraka haraka. Yehova-tsidkenu: “Yeye ni utakatifu wetu.” Mungu anapendezwa na utakatifu wangu. Anadhihirika kwa jina Yehova, anataka tuwe utakatifu wake. Anakuwa tegemeo letu, kama vile anaweka miwani machoni na anatuangalia kama vile Yesu Kristo alivyo; na anatuweka katika maisha yake ili akae ndani yetu na atusaidie kushinda mvutano wa asili yetu. Anatupa utakatifu wetu. Ndiyo maana nipinga sana kuhusu kujihesabia haki kwa wenye imani kali. Kama giza lako ni hukumu, litazame jina la Yehova-tsidkenu.

“Vema, nakaribia kupata mshangao. Na kila mara naona vitu vikija. Nashangaa, sijui ni nini hasa. Niko tu... ni mshangao wangu!” Yehova-shalom. Vuta pumza zako kabla hujaenda kwa mtaalamu wa akili na kumlipa Dola za Kimarekani 500 kwa saa kumwambia mambo yote ya nyuma uliyokosea, hivyo ilikuwa, na hii ni sasa. Hebu vuta pumzi zako ndani na kusema... jiachie kwa Bwana na kusema, “Bwana, jina lako ni Yehova-shalom.” Unasema hili linakuja na unasema hili kinakwenda: “Yeye ni amani yetu.” Anaweza kuwa kweli kama kuacha giza na kuliangalia jina lake. Biblia inasema, “Atakuagizia malaika wake wakulinde” na “atamlinda katika amani kamilifu... amani kamilifu, yeye ambaye moyo wake unamtegemea.” Ninawambie ninyi ndugu, nikiwa katika hali hii kwa muda mrefu. Ni upinzani mkubwa ambao Mungu ameweza kuudhibiti, lakini ninajua nikifanya hivi ni njia ya Mungu... (Sihubiri mawazo ya kusadikika), inafanya kazi. Yeye anaweza kuwa amani yako. Yuko pamoja nawe. Ni mkubwa kuliko matatizo yako.

“Vema, sijui hatua gani ifuatie kwenye maisha yangu. Nina maana, nina maamuzi na...” Ni watu wangapi waopatana... huna kitu chochote ambacho ni cha mafanikio? Halafu unapata njia ya mafanikio; hakuna njia, kisha kama mtu anayezama hapa linakuja koti la kuokelea na mara ghafla kwenye upande wa meli ya uokoaji wanatupa makoti arobaini mpaka naanza kuzama kwenye maji ili kukwepa yasije yakanipiga kichwani. Kisha nazama siwezi kuamua ni koti gani la kujiokoa nichukue. Pumzika. Pumzika! Mojawapo linaruka mbele ya pua yako kwa sababu Yehova-rohi. Jiachie mwenyewe kwa kutegemea, “BWANA ndiye mchungaji wangu,” Ananiongoza.

Nilihubiri hivi wiki mbili zilizopita katika mtazamo wa tofauti. Ukihubiri falsafa, baadhi ya vifungu vilivyojitenga bila, Biblia inaelezea kitu kile kile kwa njia tofauti, kwa hiyo sisi sote tunapata kitu kile kile. “BWANA ndiye mchungaji wangu”—ni mtindo wa kale wa dunia ya Mashariki ya Kati ambao mchungaji anaongoza kondoo. Hakuwaburuzi; aliwaongoza. BWANA ndiye mchungaji wangu,” Ananiongoza. Jiachie mwenyewe kwenye hilo na nenda nyumbani ukasome, Zaburi ya 23, labda maelezo ya kutuina maandiko ya kiuanadamu: “BWANA ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu.” Waebrania wanacho hicho, “Anaondoa hali ya kuwa na uhitaji, ananiandalia meza katika yangu, hataniachilia. Nguvu zetu ziko ndani yetu. Yeye ni Bwana wa majeshi, na pia ni Mungu wa maadui zetu, au machoni ya adui zangu.”

“BWANA ndiye mchungaji wangu.” Atakuongoza, lakini unatakiwa kutenda tendo fulani. Na nimesma hivi mara nyingi wiki mbili zilizopita—katika mfumo wa Agano la Jipya: unazifanya ahadi za Mungu kuwa zako. “Kwa moyo mtu huamini; kwa kichwa hukiri.” Jiachie mwenyewe kwa Mungu na useme, “Bwana ndiye mchungaji wangu. Ananiongoza. Ataninyooshea njia. Atanionyesha njia.” Sikuamini hili mwaka jana. Sikutumia muda mwingi katika jina maalumu kwa sababu sikuamini hivyo—nilitaka kufanya hivyo. Pia nilikuwa na mawazo ya ni wapi mchungaji anatakiwa kwenda, na sikuwa na ushirikiano! Nilifikiri nilikuwa na mchungaji bubu na sikuhubiri vizuri sana sehemu ya hili. Ninaweza kukukwambia leo, “Bwana ndiye mchungaji wangu.” Anaongoza; “Sitapungukiwa na kitu.” Na atakuwa mchungaji wako. Haijalishi ni tatizo gani, Ataluwa mchungaji wako.

Yehova-shammah. Napungukiwa na muda. Kama nikipungukiwa na vitu vingine, au kama nahitaji hili kabla sijahitaji vitu vingine, Yehova-shammah—“Bwana yuko pale.” Kila jina kati ya haya yalitolewa na Mungu kwa mtu aliyemchagua kuwa wake, ili awaambie ulimwengu mzima jinsi yeye alivyo. Na alichagua neno lenye maana..., kama wenye mgandamizo unaotaka kutoka, “Hivi ndivyo nitakavyoenda kujidhihirisha mwenyewe kwa watu wangu, ili kwamba mjue kilichopo wakati giza linakuja. Hii nuru iliyo kuu ya giza. Huwezi kuiona, lakini niko hapo, na nuru inang’aa. Ifikie na uikamate!”

Haya majina yote ya Yehova yanakubaliana na hali yangu kwa wakati fulani au vinginevyo, kama mengine yasipokubaliana nami, Yehova-shammah—“Mungu yuko mahali pale.” Wakati nikiwa kwenye giza, chochote ninachofanya, sehemu yoyote ninayoenda, ni yuko pale. Sielewi mfano wa kiroho wa yuko kila mahali; ninakamata hili kwa imani. Yuko pale. Siko peke yangu; Kuna—Yehova-shammah!

Nilikuwa na majina mengi zaidi—Kumbukumbu la Torati 33. Mungu anajipa jina ambalo ni la aina ya tofauti kidogo. Usiligeukie; nitakwambia baadaye. (mstari wa 16) Bwana wa majeshi ni yeye ambaye anaongelea kuhusu wimbo wa ushindi wa Musa. Na katika kipindi chote cha maisha, Musa katika Kumbukumbu la Torati 33 anatoa hotuba ya mwisho kwa watu aliowatoa kutoka kwenye vifungo, watu aliosafiri nao jangwani.

Kwa sababu walimuudhi roho—na hilo sio tatizo kwa sababu kila kiongozi lazima akutane na tatizo, walimuudhi roho wake na wakagonga mwamba mara ya pili na wakamharibu aina ya Kristo aliyekufa mara moja, alinyimwa nchi ya ahadi. Alimuomba Mungu ili aweze kwenda, na Mungu alisema,

“Hapana.” Sasa, hasira sio kitu kilichomfanya awe kwenye matatizo. Alipata hasira kwenye mlima Sinai na akavunja vibao vya mawe; lakini kwa sababu hiyo hasira yake ilileta ufunuo kwa Mungu kwa sababu ilileta aina ya Sheria ambayo ingeweza kuvunjika—Sheria inavunjwa na mikono ya wanadamu na inaweza kutunzwa kama vile ilivyokuwa kwa jozi ya pili ya mawe katika Sanduku la Agano, ambayo ni aina ya Kristo.

Hivyo hasira yake ilifanyika kuwa ufunuo kwa Mungu. Lakini wapinzani walipomuudhi roho kwa ile hasira ambayo Mungu alipomwambia “kuongea na mwamba” ambao mwanzo aliuchoma na maji yakatoka; katika hasira yake aliyapigia ukelele, “Ninyi wapinzani!” Na akaugonga. Na haikuwa hasira asilimia zote; ilikuwa ni hasira iliyosababisha yeye afanye kitu fulani ambacho kilichovunja aina fulani ya jiwe kwa sababu lile jiwe ambalo ni aina ya Kristo, lilikuwa livunjwe kwa mara moja. Hivyo aliikana nchi ya ahadi. Alisema, “Mungu, ninaweza kuiangalia tu?” Na Mungu alimtazama juu katika mlima wa Nebo na kumuacha aiangalie nchi ya ahadi, na akamkatalia kuingia. Na alikuwa na hotuba ya mwisho aliyowapa watu na ni sawa na Yehova-shammah, “Mungu yuko pale.”

Anamzungumzia Mungu anayewaongelea wao. Haongei kuhusu Mungu wa mlima Sinai ambaye alimuamuru aende pale kwenye ngurumo na kelele na radi akiandika Sheria. Hapana. Anachosema, utakuwa na “wema wake ndani ya kichaka.” Hiyo ni sehemu pekee ya Biblia... kitabu kizima; hicho ndicho kipengele pekee cha Biblia kwa tukio hilo ambapo baada ya miaka arobaini ya kondoka kwa Farao, miaka arobaini ya kufikiri aliachwa (sema na giza), miaka arobaini bila neno kutoka kwa Mungu kando ya jangwa; na ghafla yuko mbele yake, hiki kichaka kilitoa moto na haukuteketea na sauti ikasema. Na kama vile nilivyosema Jumapili au hapo nyuma kidogo, sauti haikusema, “Ninyi hapo!” Sauti haikusema, “Wewe mchungaji!”

Miaka arobaini ya kunong’ona, Mungu kwa hakika alijua ni wapi Musa alikuwa na akajitokeza katika kile kichaka na alisema, “Musa.” Alimtaja jina. Kati ya mambo yote yaliyotokea: maji matamu, yaliacha bahari ya Shamu, radi na muungurumo kwenye mlima Sinai, akiomba na kumponya ukoma Miriam, akigonnga mwamba na maji yakatoka mara ... kumbukumbu aliyokuwa nayo kwa miaka yote ambayo ingesababisha yeye kwenda kwa Mungu, na kisha kumpa jina: “Mungu wa kichaka” ilikuwa ni tukio ambalo lilimfanya ajue kwamba kamwe hakuwa nje ya uwepo wa Mungu, haijalishi kitu gani kilitokea.

Na kisha anatumia msemu “wema”—sio neno zito sana. “Kibali”..., “Neema”..., “kujifurahisha kwa”... Ni neno lenye maana mbili ambalo linatafsiriwa kama “wema”—“kujifurahisha” na “kushiriki katika maisha”. “Wema” wa Mungu unaokufurahisha na kukushishikisha katika maisha yako na kukuongoza kama ukimuomba yeye, ni “Mungu wa kwenye kichaka.” Kama ukiwa na tafsiri ya Biblia yako inayojulikana kama *26 Translation Bible*, kwamba mstari wa Kumbukumbu la Torati, sura ya 33, unaweza kuutafsiri kama, “Mungu aliyelea utukufu.” Ni saw na neno “utukufu wa *Shekinah*”, likionyesha utukufu wa Mungu. Tunaita “*Shekinah*” pale ulipokwenda kwenye Sanduku la Agano patakatifu pa patakatifu, na ruru ingeonekana pale katika siku ile ya upatanisho—Mungu akijidhihirisha mwenyewe kama nuru: *Shekinah*.

Ni nini mstari wa 16 unasema, “Mungu alikipa utukufu kichaka,” na ile tafsiri ya Biblia ya *26 Translation*, “kichaka—chenye miiba”—kibaya, kichafu, kichaka chenye miiba na vumbi. Kisichowaka na kutikisika na ngurumo na mawimbi kwenye bahari ya Sham, hicho hakigusi kwenye akili ya Musa miaka yote hiyo. “Mungu wa kichaka chenye miiba alishuka chini kwenye sehemu nyenyekevu na nje ya kichaka chenye miiba kichafu aliniita mimi kwa jina. Mungu ambaye yuko pamoja nami, Yehova-shammah”; Yuko pale siku zote. Sijali ni giza gani ulilonalo. Popote ulipo, Mungu yuko pale kwenye giza lako akikusubiri ujiachilie mwenyewe kwenye jina lako.

Sijamaliza. Kipengele cha mwisho: “Mtumaini yeye” au “ajiachilie mwenyewe... kwenye jina la Bwana, na ukae na Mungu wake.” Neno “kaa” ni neno linalotumika kama: *shaan*, mzizi wa neno *shaan*, ni “kuegemea kweye fimbo.” Nimekwambia maneno mengi ya imani, lakini ni maneno tu ya matendo. Hili neno “kaa” ni “kuegemea kwenye fimbo”; mara nyingine limekuwa likitumika katika lugha ya zamani ya wanamaji kutupa kitu na kukaa kwenye hicho kitu, lakini kimsingi ni kuegemea kwenye fimbo au msingi ambao unaweza kutegemeza kitu.

Tuna haki... ni wa Mungu kama tukiwa wakristo; lakini kwa mshangao unaweza kufunika hili ndani ya giza lako nadni ya giza langu... kama ukijitumainia mwenyewe katika jina linalokidhi mahitaji yako: kama ni kupata, Yehova –Yire; kama ni uponyaji, Yehova-rapha; kama ni kuongozwa au kuchungwa, ni Yehova-rohi, na majina yote chini mpaka kwenye Yehova-shamma: “Mungu yuko pale.”

Mungu alipotazama ule ufunuo wa Mungu katika jina kale hilo kinakidhi mahitaji yako, Biblia yangu katika mstari huu inanipa kibali cha kuufanya uwe wangu: “mtegemee Mungu.” Acha kila kitu... kama hakidhi mahitaji yako, tupilia mbali; lakini fikia mti wa Mungu wa ufunuo na kwa imani kamata jina maalumu la ufunuo linalokukidhi. Lifanye liwe lako. Uling’ang’anie! —liwe lako binafsi.

“Hili ni langu; hii ndiyo ni ahadi.” Acha kila kitu katika hilo giza kikae kando. Nina mkono wa imani katika kitu kimoja ambacho nitakaa nacho, nitakitegemea, kitanishikiza, nitajenga juu yake. Ninakifanya kiwe changu. Ninaweza kuwa wa Mungu. Lakini amenipa kibali kumfanya yeye, katika viwango maalumu, ni wangu. Yeye ni Mungu wangu... Yeye ni mali yangu... Ni mponyaji wangu... Ni mpaji wangu... Ni amani yangu... Ni utakatifu wangu... Ni mchungaji wangu... Ni uwepo wangu... Ni wangu!”

Anakuweka huru kutoka kwenye giza katika maarifa, huyu ni wangu na ninadai hili, na kama nikifa nikining’inizwa juu na msumari kidoleni, nitaamka pale ambapo hakuna mawingu mbele ya nuru. Huu ndiyo ujumbe wangu kwa leo.

haki © 2007, Mchungaji Melissa Scott. – Haki zote zimehifadhiwa